IKULU
ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 030 ISSN 1821 - 8253 DISEMBA 2016

RISALA YA MWAKA MPYA 2017 DK. SHEIN AMESEMA

- Uchumi umeendelea kuimarika
- Washirika wa maendeleo wameendelea kuonesha imani yao kwa Serikali

Website: www.ikuluzanzibar.go.tz / Email: info@ikuluzanzibar.go.tz / Twitter: Zanzibarupdates / Facebook: Zanzibarupdates

Maoni ya Mhariri

Hatimaye tumepata tulichokitaka

Tarehe 15 Novemba, 2016 Zanzibar iliandika tena katika vitabu vya historia yake tukio kubwa ambalo bila ya shaka yoyote limeleta matumaini mapya na makubwa ya kujenga mustakbala mwema na imara wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Zanzibar kwa miaka mingi ijayo.

Ni tukio la kuhitimisha mchakato wa muda mrefu wa kutunga Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar ambao umekamilishwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa kutia saini Sheria hiyo Namb. 6 ya mwaka 2016 mbele ya viongozi mbali mbali wa Serikali na waandishi wa habari.

Sheria hii inaipa Zanzibar mamlaka ya kutafuta na kuchimba mafuta na gesi asilia ambayo hapo awali haikuwanayo kutokana na sheria zilizokuwepo kuipa mamlaka hayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika lake la uchimbaji mafuta TPDC pekee.

Ni ukweli kuwa hadi kufikia hatua ya kutiwa saini sheria hiyo kulikuwepo na mazungumzo ya muda mrefu kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu suala la mafuta na gesi kuondolewa katika orodha ya mambo ya Muungano.

Ni kitu cha kujivunia na kumshukuru Mwenyezi Mungu kuwa mashauriano hayo yalifanyika katika mazingira ya udugu, urafiki na mshikamano ambao lengo lake lilibaki katika kutafuta mustkabala mwema wa watu wa pande mbili hizi za muungano.

Kwa hivyo ni wajibu wetu kuwashukuru viongozi wetu waliosimamamia suala hili hadi kufikia hatua ambayo wananchi wa Zanzibar wamepata na kuridhika na kile ambacho walikuwa wakikililia kwa miaka mingi.

Hatuna budi kuwashukuru viongozi wetu wa kitaifa kwa busara zao hadi kufikia hatua hii. Tunampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake imara uliojaa busara, hekima na uvumilivu na zaidi imani yake katika uongozi wa pamoja ambapo hata wakati mmoja katika masuala makubwa ya nchi hakuacha kuwashirikisha viongozi kupitia kwenye vikao rasmi vya maamuzi.

Safu hii ya Mhariri inaamini kwa dhati kabisa kwa kuwa changamoto ni suala la lazima katika mchakato wa maendeleo, zilikuwepo changamoto kadhaa katika hatua za mashauriano, lakini busara umahiri na umakini mkubwa wa Dk. Shein katika uongozi hatimae imefikiwa hatua ya kutiwa saini sheria hiyo tukio ambalo limepokelewa kwa shangwe na vigelegele na wananchi wa Zanzibar hasa wapenda maendeleo.

Aidha, ni wajibu wetu pia kumshukuru kwa namna ya pekee Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Jakaya Mrisho Kikwete kwa busara zake na uongozi wake thabiti katika kulishughulikia jambo hili.

Utayari wake tu ndio uliowezesha jambo hili kufanyika kwa namna lilivyofanyika. Angeweza, kwa wakati aliokuwepo, kusema suala hili aliahirishe limsubiri Rais ajaye kwa vile liliendelea hadi karibu na kufikia ukingoni mwa uongozi wake. Alitumia busara ya kiuongozi pamoja na uungwana kwa kuangalia haja na mahitaji ya ndugu zake wa Zanzibar katika kujenga na kuimarisha uchumi wao.

Dk. Kikwete alielewa fika kuwa 'fursa haiji mara mbili' hivyo ilikuwa ni wakati muafaka kwake kuuharakisha mchakato ule hadi Bunge likapitisha Sheria Mpya ya Mafuta Namb. 21 ya mwaka 2015 ambayo inaipa uwezo Zanzibar kushughulikia masuala ya mafuta na gesi asilia kwa kutumia sheria itakazozitunga yenyewe. Katika mtazamo huo huo, Dk. Kikwete hakufanya ajizi akatia saini Sheria hiyo tarehe 5 Agosti, 2015.

Zanzibar sasa ina sheria yake ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa lugha za wenzetu wanasema sasa "mpira uko upande wetu". Tunatakiwa kuucheza! Kwa bahati nzuri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianza matarayarisho ya kuendeleza sekta hii muda mrefu baada ya kupata matumaini ya kuwepo mazingira ya sasa ya kuwa na sheria yake. Sera ilikwishaundwa na kupitishwa.

Ni kweli kuwa Sheria hii imeleta matumani kwa kila mwananchi wa Zanzibar lakini kama alivyotahadharisha Mheshimiwa Rais baada ya kusaini sheria hii kuwa isitegemewe kuwa manufaa ya sekta ya mafuta na gesi yatapatikana kufumba na kufumbua. La hasha, inaweza kuchukua miaka isiyopungua kumi lakini kubwa alilosisitiza ni ustahamilivu tena si kwa wananchi tu lakini hata kwa serikali yenyewe!

Alichomaanisha Mheshimiwa Rais ni kuwa bado kuna safari ndefu hadi kufikia hatua ya kufaidika na sekta hii na hata Sheria yenyewe inathibitisha hilo kwani inaanza na neno "kutafuta", ikimaanishwa kutaka kitu au jambo ambalo hulijui lilipo. Hivyo sijambo lililo tayari!

Bodi ya Wahariri

Mhariri Mkuu
Hassan K. Hassan

Mhariri Msaidizi
Said J.Ameir

Waandishi
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

Mpiga Picha
Ramadhan O. Abdalla

Msanifu
Aziz I. Suwed

UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.

Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

P.O.BOX: 2422

Zanzibar - Tanzania

Phone: +255 223 0814/5

Fax: 024 223 3722

Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz

1

RISALA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI DK. ALI MOHAMED SHEIN YA KUUKARIBISHA MWAKA MPYA 2017

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amesema katika kipindi cha mwaka 2015 Uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika na washirika wa maendeleo wameendelea kuonesha imani yao kwa serikali kwa kuchangia fedha za kutekelezea miradi mbali mbali ya maendeleo.

Katika risala yake ya kuukaribisha mwaka 2017, Dk. Shein amesema kwa mwaka 2015, Pato Halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 6.6. Hadi kufikia robo mwaka ya pili (Aprili - Juni) mwaka 2016 uchumi umekua kwa kasi ya asilimia 6.2. Aidha, Serikali imefanikiwa kuongeza kiwango cha kukusanya kodi ambapo katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2016 imeweza kukusanya jumla ya TZS bilioni 441.3 kutokana na vyanzo vyetu vya ndani.

Kiasi hicho ni kikubwa ikilinganishwa na mwaka wa nyuma katika kipindi kama hicho, ambapo Serikali ilimudu kukusanya TZS bilioni 336.6. Hii ina maana kwamba kwa miezi kumi ya mwanzo ya mwaka 2016, mapato ya Serikali yameongezeka kwa TZS bilioni 104.7 sawa na ukuaji wa asilimia 31.1. Sambamba na mafanikio hayo, washirika wa maendeleo wameridhika na juhudi za Serikali na hivyo kuendelea kusaidia miradi ya maendeleo.

Amesema katika kuthibitisha imani ya washirika wa maendeleo kwa Serikali, SMZ imepokea jumla ya TZS bilioni 54.53 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kati ya mwezi wa Januari hadi Oktoba, 2016. Kiasi hicho ni kikubwa ikilinganishwa na TZS bilioni 47.47 ambazo Serikali ilizipokea katika kipindi kama hicho mwaka 2015 tulipokea. Fedha hizo ni sawa na ongezeko la asilimia 14.9.

Ifuatayo ni risala kamili ya Rais wa Zanzibar aliyoitoa kwa wananchi wakati alipokuwa akiwasilisha kwa wananchi kupitia vyombo vya habari.

Dk. Ali Mohamed Shein
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Assalamu Aleikum Warahmatullah Wabarakatuh

Ndugu Wananchi,

Tuna wajibu mkubwa wa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muweza wa kila jambo kwa kuturuzuku neema ya uhai tukaweza kuifikia siku hii tunapouaga mwaka 2016 Miladiya na kuukaribisha mwaka mpya wa 2017. Hapana shaka, kwamba tuliuanza mwaka 2016 tukiwa na wenzetu ambao kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu, wameshatangulia mbele ya haki. Tumuombe Mola wetu awape malazi mema peponi na sisi tulio hai atujaalie kila la kheri katika maisha yetu hapa duniani na atupe hatma njema. Amin!

Ndugu Wananchi,

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu; Subhana Wataala kwa kutuwezesha kuyakabili kwa mafanikio makubwa masuala mbali mbali tuliyoyatekeleza katika mwaka 2016, ambao sasa tunaouaga. Mtakumbuka kwamba miongoni mwa matukio makubwa ya mwaka 2016, ni kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu wa tarehe 25 Oktoba, 2015 ambao ulifutwa na Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar pamoja na matokeo yake. Uchaguzi huu ukarudiwa tena tarehe 20 Machi, 2016.

Katika uchaguzi huo wananchi walishiriki kupiga kura kwa amani na kuitumia vyema haki ya kidemokrasia na kikatiba ya kuwachagua viongozi wanaowataka. Kwa mara nyengine wananchi mlionesha imani yenu kwa Chama cha Mapinduzi na mimi mkanichagua kwa asilimia 91.4 na vile vile, mmewachagua wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM.

Uamuzi wenu huo mmeiwezesha CCM kuunda Serikali, pamoja na kupata idadi kubwa ya Wajumbe wa Baraza la Tisa la Wawakilishi na Baraza hilo nililizindua tarehe 05 Aprili, 2016. Kwa niaba ya viongozi wenzangu wote

kwa mara nyengine tunatoa shukurani zetu kwenu na kuahidi kukutumikieni kwa uwezo wetu wote.

Ndugu Wananchi,

Katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja, wa uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Saba, kwenye kipindi hiki cha pili, nchi yetu imepata mafanikio ya kuridhisha katika utekelezaji wa mipango yetu mikuu ya maendeleo ikiwemo Dira ya Maendeleo ya mwaka 2020, MKUZA, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 pamoja na mipango mingine ya kisekta.

Tathmini tuliyoifanya hadi tunapouaga mwaka 2016 na kuukaribisha mwaka mpya wa 2017, inaonesha tumeweza kupiga hatua katika malengo yetu ya kuinua uchumi na kuimarisha huduma za jamii, zikiwemo afya, elimu na huduma za maji safi na salama na nyenginezo.

Ndugu Wananchi,

Uchumi wetu umeendelea kuimarika. Kwa mwaka 2015, Pato Halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 6.6. Hadi kufikia robo mwaka ya pili (Aprili - Juni) mwaka 2016 uchumi umekua kwa kasi ya asilimia 6.2. Kadhalika, tumefanikiwa kuongeza kiwango cha kukusanya kodi. Kwa kipindi cha Januari hadi Novemba, 2016 Serikali imeweza kukusanya jumla ya TZS bilioni 441.3 kutokana na vyanzo vyetu vya ndani.

Kwa kipindi kama hicho mwaka jana (2015) tulimudu kukusanya TZS bilioni 336.6. Hii ina maana kwamba kwa miezi kumi ya mwanzo ya mwaka 2016, mapato yetu yameongezeka kwa TZS bilioni 104.7 sawa na ukuaji wa asilimia 31.1. Sambamba na mafanikio hayo, washirika wetu wa maendeleo wameithamini sana kazi nzuri tunayoifanya ya kuwaletea maendeleo wananchi.

Katika kuthibitisha imani yao kwetu, Serikali imepokea jumla ya TZS bilioni 54.53 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kati ya mwezi wa Januari hadi Oktoba, 2016. Kipindi kama hicho kwa mwaka 2015 tulipokea TZS bilioni 47.47, sawa na ongezeko la asilimia 14.9. Huu ndio ukweli halisi na hio ndiyo hali halisi ambayo ni vyema wananchi mkaifahamu kuwa ni nzuri; kinyume na maelezo yanayotolewa na baadhi ya watu ambao hawana taarifa sahihi na takwimu za uhakika za Serikali yetu. Tutajidhatiti zaidi katika mwaka ujao na Mwenyezi Mungu akipenda mambo yatakuwa bora zaidi.

Ndugu Wananchi,

Kwa upande wa huduma za jamii mwaka unaomalizika, utakumbukwa kwa hatua za mafanikio tuliyoyapata katika kuimarisha huduma za afya nchini. Tarehe 11 Novemba, 2016 tulizindua majengo ya wodi mpya ya watoto na wodi ya wazazi katika hospitali kuu ya Mnazi mmoja. Wodi hizo zimetiwa vifaa vya kisasa vya kutolea huduma, na kuwa na nafasi ya kutosha kwa wagonjwa watakaofika kuhudumiwa. Hii ni hatua muhimu katika utekelezaji wa lengo la Serikali la kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa hospitali ya rufaa kamili na kuimarishwa kwa huduma zake.

Kadhalika, tarehe 26 Novemba, 2016 tulifanya uzinduzi mwengine nao ni wa Hospitali ya Abdalla Mzee, Mkoani Pemba baada ya kujengwa upya kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Kufunguliwa kwa hospitali ya Abdalla Mzee ambayo sasa imefikia hadhi ya Hospitali ya Mkoa kutawawezesha wananchi wa Pemba kupata huduma mbali mbali za afya ambazo mwanzoni walilazimika kuzifuata nje ya Kisiwa cha Pemba.

Dhamira ya Serikali ni kuyaendeleza mafanikio hayo katika mwaka ujao, kwa kuzidi kuchukua hatua ili huduma za afya nchini ziimarike zaidi na ziwe za viwango bora. Maelekezo ya kina ya mafanikio tuliyoyapata kwa kila sekta, penye majaaliwa nitayatoa katika hotuba yangu ya kilele cha maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ifikapo tarehe 12 Januari, 2017.

Ndugu Wananchi,

Kwa lengo la kuwaenzi wazee wetu na kuthamini mchango wao katika maendeleo ya nchi yetu, Serikali, katika mwaka unaomalizika, ilianza utekelezaji wa Mpango wa Pencheni ya Jamii. Kupitia mpango huu wazee wote waliofikia umri wa miaka 70 na kuendelea waliosajiliwa, wameanza kupewa posho la TZS 20,000 kwa mwezi. Kuanzia mwezi Aprili 2016, tulipoanza utaratibu huu, idadi yao imeongezeka kutoka watu 21,263 waliosajiliwa mwaka 2015, hadi kufikia watu 26,603 mwezi wa Novemba, 2016.

Hivi sasa Serikali inaendelea kuwasajili watu wengine waliotimiza sifa za kuwemo katika mpango huo ambao hapo mwanzo hawakusajiliwa. Vile vile tutazifanyia kazi changamoto zilizojitokeza kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mpango huo. Kadhalika, Serikali inazingatia haja ya uwezekano wa kuongeza idadi ya wazee wanaopaswa kuwemo kwenye mpango huu, kwa kupunguza umri hadi kufikia miaka 65 badala ya miaka 70 kama ilivyo hivi sasa. Vile vile, tunazingatia haja ya kuwaandalia wazee huduma za afya kwa dhamira ile ile ya kuwatunza na kuwaenzi wazee wetu.

Ndugu Wananchi,

Tukio jengine mahususi katika mwaka tunaoumaliza lilikuwa ni kutiwa saini kwa Sheria Namba 6 ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2016 inayoipa Zanzibar uwezo wa kisheria wa kushughulikia utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Hili ni tukio kubwa, ambalo kwa umuhimu wake tuliamua kulifanya hadharani hapo tarehe 15 Novemba, 2016, kwenye ukumbi wa Ikulu, mbele ya viongozi mbali mbali, wafanyakazi, wananchi na wafanyakazi wa vyombo vya habari.

Kufuatia hatua hii, Zanzibar imepata uwezo wa kisheria wa kushughulikia utafutaji na uchimbaji wa rasilimali hizi muhimu ili nazo ziweze kuchangia pato la uchumi wetu. Hadi sasa mipango yetu katika suala hili inaendelea vizuri. Tunaendelea na mazungumzo na baadhi ya wawekezaji wenye uwezo mkubwa na uzoefu wa masuala ya mafuta na gesi asilia ambao wana nia ya kuwekeza nchini kwetu.

Ndugu Wananchi,

Katika mwaka tunaoumaliza, Serikali iliendelea kufanya jitihada katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira nchini kama ilivyo kwa

mataifa mengine duniani. Katika jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia Mfuko wa Uwezeshaji kwa kutoa mikopo kwa wananchi wanaojishughulisha na biashara, kilimo, uvuvi, ufugaji na nyenginezo, vile vile, Serikali iliandaa Kongamano na maonesho ya Wajasiriamali tarehe 03 Disemba, 2016 na tarehe 04 Disemba, 2016 ambapo maonyesho hayo yalifanyika katika jengo la zamani la Baraza la Wawakilishi Kikwajuni.

Lengo la kongamano na maonesho hayo lilikuwa ni kutoa fursa kwa wajasiriamali kujifunza mbinu bora za kufanya shughuli zao ili kuongeza tija. Aidha, shughuli hiyo ilikuwa na lengo la kuongeza hamasa na taaluma, hasa kwa vijana ili waweze kuzifahamu fursa ziliopo katika ujasiriamali, kwa lengo la kujiajiri wenyewe na kuondokana na hisia za kutegemea ajira chache zinazopatikana Serikalini.

Katika mwaka ujao, Serikali itaendeleza jitihada za kuwasaidia wajasiriamali kwa kuwapatia fursa zaidi za mikopo, kutafuta masoko ya bidhaa zao na kuwapa mafunzo kwa njia ya mafunzo mbali mbali, zikiwemo semina na makongamano pamoja na kukiendeleza kituo cha kukuza na kulelea Wajasiriamali, kilichopo Mbweni.

Ndugu Wananchi,

Katika kuimarisha Maadili ya Viongozi na utawala bora, Serikali katika mwaka 2016 ilikamilisha uundaji wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo tayari imeshaanza kufanya kazi zake. Madhumuni ya kuchukua hatua hizo ni katika utekelezaji wa matakwa ya kisheria kwa mujibu wa sheria ya Maadili Namba 4 ya mwaka 2015. Miongoni mwa majukumu ya Tume ya Maadili ni kuhakikisha kwamba viongozi wa umma na wale wote waliotajwa katika sheria ya Maadili, wanajaza fomu ya tamko la rasilimali na madeni ambazo tayari zimekwishatolewa kwa wahusika na kutakiwa kuzirejesha Tume fomu hizo, si zaidi ya tarehe 31 Disemba, 2016.

Napenda nisisitize kauli yangu niliyoitoa tarehe 10 Disemba, 2016 katika maadhimisho ya siku ya Maadili kwenye viwanja vya bustani ya Victoria, ya kuwataka wanaohusika wote wazingatie maelekezo yaliyotolewa kwenye fomu hio na waepuke kutoa taarifa zisizo za kweli, kwani kufanya hivyo ni kitendo cha kuvunja maadili ya uongozi.

Aidha, nahimiza kuwa kila mmoja wetu azingatie kauli mbiu ya maadhimisho ya siku ya maadili isemeyo: “Imarisha utawala bora kwa kukuza uadilifu, uwajibikaji, haki za binadamu na mapambano dhidi ya rushwa.” Huo ni ujumbe muhimu wa kuuzingatia wakati tunapouanza mwaka mpya wa 2017. Sote tuazimie kuitekeleza kauli hii kwa vitendo, kwani nchi yetu inaongozwa kwa kufuata sheria na misingi hiyo muhimu ya utawala bora.

Ndugu Wananchi,

Katika kusherehekea kumalizika kwa mwaka huu na kuja kwa mwaka mpya, wapo baadhi ya watu ambao husherehekea kwa vitendo ambavyo huweza kuharibu amani na utulivu na kusababisha usumbufu kwa watu wengine. Ni vyema sote tuzingatie umuhimu wa kuitunza amani, umoja na mshikamano wetu kwani ndiyo msingi wa mafanikio tunayoendelea kuyapata katika nyanja za uchumi, siasa na ustawi wa jamii. Kwa hivyo, kila mmoja wetu ana jukumu la kudumisha amani kwani Serikali haitosita kumchukulia hatua mtu yeyote au kikundi chochote kitakachofanya vitendo vinavyohatarisha amani na usalama wa wananchi na mali zao pamoja na wageni wanaoitembelea nchi yetu.

Ndugu Wananchi,

Wakati tunauaga mwaka 2016 na kuukaribisha mwaka 2017, nchi yetu bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali, zikiwemo athari za mabadiliko ya tabianchi, zinazoathiri ufanisi katika utekelezaji wa mipango yetu ya kiuchumi na maendeleo. Tuna changamoto ya ukosefu wa ajira hasa kwa vijana na tatizo la kuendelea kuwepo kwa vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Taarifa kutoka katika Jeshi la Polisi Zanzibar zinaonesha kuwa idadi ya makosa ya udhalilishaji wa kijinsia, yaliyoripotiwa katika vituo vya Polisi, yameongezeka kutoka makosa 169 mwaka 2015 hadi kufikia makosa 512, kati ya Januari hadi wiki ya pili ya Disemba, 2016 sawa na ongezeko la asilimia 203. Hii si taarifa nzuri. Natoa wito kwa wananchi wote tushirikiane katika kuvikomesha vitendo vya udhalilishaji. Ni dhahiri kuwa ufumbuzi wa changamoto hizi unahitaji mchango wa kila mmoja wetu na sio Serikali peke yake.

Sote tuna wajibu wa kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo pamoja na kutii sheria bila ya kushurutishwa. Mafanikio yetu ya sasa na yale ya baadae yanategemea sana ushirikiano na umoja wetu, katika kujenga nchi yetu. Mambo hayo muhimu yawe ndiyo dira yetu. Ni jukumu letu sote kwa pamoja na lazima tutimize wajibu wetu huo.

Ndugu Wananchi,

Kwa kumalizia risala yangu hii, napenda nikukumbusheni kwamba tarehe 12 Januari, 2017, tunaadhimisha Miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Sote tuna wajibu wa kuyasherehekea na kuyadumisha Mapinduzi kwani ndiyo yaliyotukomboa. Wito wangu kwenu ni kwamba kila mmoja wetu ajitahidi kushiriki katika maadhimisho yetu hayo yanayotanguliwa na shamra shamra mbali mbali za uzinduzi wa miradi ya maendeleo kwa uwekaji wa mawe ya msingi. Aidha, jambo hili litaongeza chachu ya sherehe zetu tutakaposhiriki katika siku ya kilele kwenye Uwanja wa Amaan ili kuzifanikisha sherehe hizi adhimu na muhimu.

Namalizia risala yangu kwa kutoa salamu za mwaka mpya kwa wananchi wote wa Zanzibar, Tanzania Bara, ndugu na marafiki wote popote walipo. Kadhalika, natoa salamu kwa viongozi wa nchi marafiki, Taasisi za kimataifa na washirika wetu mbali mbali wa maendeleo. Mola wetu aujalie kheri na baraka nyingi mwaka mpya wa 2017. Aiongezee nchi yetu amani, umoja, mshikamano na mapenzi baina yetu. Mwenyezi Mungu atupe uwezo wa kuitekeleza mipango yetu ya maendeleo kwa ufanisi mkubwa.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza

2

Mafanikio ya sekta ya ujasiriamali Zanzibar

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi zawadi Ofisa wa Taasisi ya 'Mlele Zanzibar Foundation' hapa Zanzibar Eshe Haji Ramadhan katika hafla ya uzinduzi wa Kongamano la Wajasiriamali Zanzibar katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la zamani Mnazi Mmoja Mjini Unguja, tarehe 03 Disemba, 2016

Dalili za mafanikio ya jitihada za serikali katika kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana nchini zimeanza kuonekana kutokana na vijana wengi kuanza kubadili ufahamu wao wa awali kwamba serikali ndio chombo pekee chenye uwezo wa kutoa ajira kwa wananchi wake.

Dhana hiyo ambayo siyo sahihi ilijengeka miongoni mwa wananchi wengi wa Zanzibar wakiwemo wazee, vijana wanawake na wanaume na kwa muda mrefu athari yake imekuwa ndio chanzo cha kuwa na watu wengi tegemezi na hivyo kurejesha nyuma juhudi za serikali za kukuza uchumi wa taifa.

Ni jambo la faraja na kutia moyo kuona kwamba kwa kadiri siku zinavyokwenda, wananchi wengi ndivyo wanavyoendelea kutambua umuhimu wa shughuli za ujasiriamali na kuondokana na mtazamo uliokuwa umejengeka ndani ya jamii kwamba ajira lazima iwe ile ya kutoka serikalini au taasisi maalumu inayotambulika sana kitaifa au kimataifa.

Katika kuthibitisha kuwa dhana hiyo haikuwa sahihi, kumekuwa na wimbi kubwa la vijana waliohamasika kujiingiza katika shughuli za ujasiriamali mara tu wanapolamiza masomo yao ya vyuo vikuu. Lakini wingi wa vijana walioshiriki kwenye Kongamano la wajasiriamali lililofanyika hivi karibuni katika ukumbi wa zamani wa Baraza la Wawakilishi Kikwajuni unathibitisha mwamko ambao wananchi na hasa vijana wameanza kuupata kuhusu umuhimu wa shughuli za ujasiriamali.

Uzoefu wa hivi karibuni unaonesha kuwa vijana wenye elimu ya juu ndio wahusika wakuu kwenye shughuli za ujasiriamali jambo ambalo ni tofauti na miaka iliyopita wakati vijana wengi wasomi walikuwa wakitegemea ajira chache zilizokuwa zikitolewa serikalini.

Idadi kubwa ya vijana na hasa wanawake wanaojiunga kwenye kituo cha kulelea wajasiriamali inadhihirisha pia mwamko wa vijana katika kujiajiri. Takwimu za kituo cha kukuzia na kulelea wajasiriamali Zanzibar (ZTBI) zinaonesha kuwa idadi ya wajasiriamali ambao wameshapatiwa mafunzo kwenye chuo hicho imeshafikia wajasiriamali 764 kutoka mwezi Januari mwaka 2015 hadi mwezi Novemba mwaka 2016.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akizindua Kongamano la Wajasiriamali katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la zamani Mnazi Mmoja Mjini Unguja, tarehe 03 Disemba, 2016

Asilimia kubwa ya vijana wanaojiunga na kituo hicho ni wanawake ambao ni asilimia 86, na aslimia 14 ni wanaume.

Ni dhahiri kwamba hatua hiyo ni mafanikio makubwa kwa serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 imejipangia kufanya shughuli mbali mbali za kuinua uchumi na kuondokana na umasikini ikiwemo kuendelea kuimarisha Mfuko wa Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ili kuongeza uwezo wake wa kutoa mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo, kuimarisha kituo cha kulelea wajasiriamali na kuendelea kutoa mafunzo mbali mbali ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri vijana na kuondokana na umasikini.

Kwa upande mwengine, dhamira ya serikali katika kuendeleza ujasiriamali nchini imeonekana kwenye mipango yake mbali mbali ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Kwa mfano malengo ya Dira ya 2020 ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yameeleza wazi dhamira yake ya kukuza ujasiriamali na ubunifu.

Aidha, Sera na mipango mbali mbali ya Serikali imeweka umuhimu wa kuwaendeleza wajasiriamali ikiwa ni pamoja na Sera ya Sekta isiyo Rasmi "MSEMEs Policy" ya mwaka 2005, sera ya ajira ya mwaka 2009, Mpango wa utekelezaji wa Ajira kwa Vijana wa mwaka 2014 hadi 2018 pamoja na uamuzi wa Serikali wa kuanzisha kituo cha kulea na kukuzia Wajasiriamali Zanzibar kilichoko Mbweni.

Itakumbukwa kwamba katika kuhakikisha kuwa azma ya serikali ya kuinua sekta ya ujasiriamali inafanikiwa, tarehe 21 Disemba, 2013 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, alizindua Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ukiwa na jumla ya TZS bilioni 2.3.

Mfuko huu ulichukua nafasi ya mifuko ya aina hii iliyotangulia ikiwa ni pamoja na Mfuko wa AK/JK na Mfuko wa Kujitegemea. Majukumu makubwa ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni kuwapatia wananchi huduma za kifedha ili waweze kufanya shughuli za uzalishaji kwa lengo la kunyanyua hali zao za maisha.

Vile vile, Mfuko huu una jukumu la kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kuongeza fursa za ajira hasa kwa vijana, wanawake na makundi maalum.

Ni jambo la kutia moyo kuona kuwa Mfuko huu umepata mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano katika kipindi cha miaka miwili na miezi minne tangu Mfuko huu kuanza kazi zake, yaani kuanzia Julai 2014 hadi Oktoba 2016, jumla ya mikopo 998 yenye jumla TZS 1,687,410,000/= imeshatolewa Unguja na Pemba kwa wananchi wanaofanya shughuli mbali mbali zikiwemo biashara, wakulima, wavuvi, wafugaji na wengineo. Jambo la kufurahisha ni taarifa zinazoonesha kwamba asilimia 67 ya watu waliopatiwa mikopo ya Mfuko huu ni vijana wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35.

Lakini sifa moja kubwa ambayo wajasiriamali wa Zanzibar wanapaswa kupewa ni kitendo chao cha kukopa bila ya kusahau kulipa. Takwimu zinaonesha kuwa kuanzia mwezi Julai 2014 hadi Oktoba 2016, jumla ya TZS 991,986,705/= ambazo zilikopwa zimerejeshwa. Katika fedha hizo TZS 403,693,905/= zimerejeshwa mwaka 2014/2015, TZS 435,644,500/= zimerejeshwa mwaka 2015/2016 na TZS 152,648,300/= zimekusanywa katika kipindi cha miezi minne ya Julai hadi Oktoba, 2016. Marejesho hayo ni wastani wa asilimia 96 ya makadirio ya makusanyo.

Hali hiyo ni tofauti na wakopaji wa miaka ya nyuma ambao waliichukulia mikopo waliyokuwa wakipewa kama ni sadaka ambayo haipaswi kurejeshwa.

Uamuzi wa serikali wa kuelekeza nguvu zake kwa wajasiriamali unatokana na uzoefu wa mataifa yaliyoendelea ambayo mafanikio yao makubwa yamepatikana kutokana na nchi hizo kuwajengea mazingira mazuri wananchi wake walioamua kujiingiza katika shughuli za ujasiriamali. Aidha, dunia imeweka mifano ya watu na taasisi zilizoanzishwa katika utaratibu wa ujasiriamali na hatimae kupata mafanikio ya kupigiwa mfano.

Kadhalika, miongoni mwa wafanyabiashara wakubwa nchini Tanzania ni wafanyabiashara ambao wameanza shughuli za ujasiriamali kabla ya kuwa wafanyabiashara mashuhuri nchini.

Waliofanikiwa katika shughuli za ujasiriamali wametafsiri kwa vitendo dhana ya ujasiriamali kwamba ni kuwa na ujasiri katika kutafuta mali, lakini kwa njia za halali. Hii ni kwa mujibu wa mwana uchumi wa Australia Joseph Schumpeter ambaye ameutafsiri Ujasiriamali kuwa ni utaratibu na uendeshaji wa shughuli za kibiashara kwa ubunifu kwa lengo la kupata faida na kuwa tayari kukabiliana na hasara yoyote itakayojitokeza.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyu wa uchumi, mjasiriamali lazima awe na mipango madhubuti ya uendeshaji wa shughuli yake ya kiuchumi, awe na ubunifu kwa azma ya kupata faida ya biashara yake lakini zaidi kuliko yote asiogope vikwazo au changamoto ambazo anaweza kukabiliana nazo ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kupata hasara.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali zenye lengo la kuwaondoshea vikwazo wajasiriamali ikiamini kwamba njia hiyo siyo tu italisaidia taifa kuondokana na changamoto ya ajira, lakini pia itasaidia katika mapambano yake dhidi ya umasikini na hatimaye kukuza uchumi wake.

Kadhalika Serikali inafahamu kwamba ujasiriamali ni jambo kubwa duniani ambalo limeweza kubadilisha maisha ya watu wengi kutoka hali ya umasikini na kuwafanya wawe na kipato kikubwa. Jambo linalohitajika ni watu kuwa wabunifu na majasiri wa kuzitumia fursa mbali mbali zilizomo katika jamii na mazingira yaliyopo. Sambamba na hilo, jamii inatakiwa kuwa tayari kujifunza kutoka kwa wale waliofanikiwa.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi zawadi Meneja wa Tawi la DTB hapa Zanzibar Mbarouk Ramadhan Mbarouk katika hafla ya uzinduzi wa Kongamano la Wajasiriamali Zanzibar, tarehe 03 Disemba, 2016

Akifungua kongamano la siku mbili la wajasiriamali, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amesema Serikali imedhamiria kubadilisha mitaala katika Skuli za Sekondari sambamba na kuimarisha vyuo vya amali. Lengo la mkakati huo ni kuona kuwa somo la ujasiriamali linachukua nafasi kubwa kwenye mitaala ya skuli ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapomaliza masomo yao ya sekondari wanakuwa na uelewa kuhusiana na masuala ya ujasiriamali na hivyo inawafanya kuwa rahisi kwao kujiajiri wenyewe.

Rais wa Zanzibar ametoa wito kwa wajasiriamali kujipa matumaini na kujifunza kutoka kwa watu matajiri na maarufu duniani kote ambao chanzo chao kimetokana na shughuli za ujasiriamali. Matajiri kama vile Bill Gate, Mwanzilishi wa Kampuni ya Microsoft kutoka Marekani, Mark Zuckerberg, ambae naye Mjasiriamali wa mitandao na Mwanzilishi wa Kampuni na Mtandao wa Facebook ni watu mashuhuri duniani ambao biashara zao zilianzia na ujasiriamali. Kadhalika mfanyabiashara maarufu Tanzania na duniani kote Bwana Said Salim Bakhressa Mwanzilishi wa Kampuni ya Azam Marine hapa nchini ameanza na shughuli ndogo ndogo za ujasiriamali hadi kufikia hatua ya sasa.

"Mtajifunza mengi ya kutia moyo na kusisimua kutokana na historia za watu hao na maendeleo waliyopata kwa ujasiri na ubunifu wao katika shughuli za ujasiriamali. Kwa hivyo, nakuhimizeni muendelee kukuza vipaji na elimu mlizonazo mkiamini kwamba nanyi mnaweza kufaidika kama walivyofanikiwa wao". Alisema Dk. Shein.

"Jifunzeni kwa wenzenu kutoka nchi mbali mbali hasa India, ambapo vijana wengi waliosoma wamekuwa wakijiajiri wenyewe baada ya kumaliza masomo yao, hususan katika sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Hivi sasa, kupitia mitandao vijana wengi wamekuwa wakichukua kazi kutoka nchi mbali mbali za Ulaya na Amerika, wanazifanya wakiwa India kwa njia ya mitandao online jobs" Aliongeza.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alitoa pongezi maalum kwa Dr. Rajeev Aggarwal kutoka India kwa juhudi zake anazozichukua katika kukiongoza na kukiendeleza kwa mafanikio makubwa kituo cha kulea na kukuzia Wajasiriamali kilichoko Mbweni.

Ameiagiza Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kuharakisha ujenzi wa kituo kama hicho Pemba ili wajasiriamali wa huko nao waweze kufaidika na huduma hizo.

3

SMZ imekamilisha kuweka misingi ya utawala bora Zanzibar

Mpango wa muda mrefu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wa kuweka misingi imara ya kutekeleza utawala bora umekamilika kufuatia kukamilishwa uundwaji wa taasisi za uwajibikaji.

Mpango huo ambao unalenga katika kuimarisha utawala wa sheria na uwajibikaji ulianza kutekelezwa tokea mwanzoni mwa mwaka 2000 na umekamilika mwanzoni mwa kipindi cha pili cha awamu ya saba ya uongozi kinachoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein baada ya kupitishwa sheria Nam 4 ya Maadili ya viongozi Umma.

Historia inatufundisha kuwa, kwa namna na nyakati tofauti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu zote, imekuwa ikiunda na kuziendeleza taasisi mbali mbali zenye kushughulikia na kusimamia suala la utawala bora.

Itakumbukwa kuwa Serikali iliunda Wizara inayoshughulikia masuala ya Utawala Bora mwaka 2000, ikaanzisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Idara ya Utawala Bora, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi na hivi karibuni Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Vile vile, juhudi kubwa zimechukuliwa za kuiimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Sheria ya Utumishi wa umma nayo imeweka bayana haki na wajibu wa watumishi wa umma katika kutekeleza majukumu yao.

Kwa madhumuni hayo hayo, Serikali imeanzisha utaratibu wa kuziita Ikulu Wizara zote za Serikali kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Mpango Kazi kila baada ya robo mwaka kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na utawala bora na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akizungumza na Viongozi na Wananchi katika sherehe za Maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu Duniani zilizofanyika katika viwanja vya Victoria Garden Mjini Unguja, tarehe 10 Disemba 2016

Masuala ya haki za binadamu ambayo imekuwa agenda kubwa kitaifa na kimataifa, yamewekwa chini ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Sheria maalum iliyoipa mamlaka Tume hiyo kufanya kazi Zanzibar mwaka 2003. Tume hiyo ilianza kufanya kazi rasmi Zanzibar mwaka 2007.

Maadhimisho ya siku ya maadili yaliyofanyika Bustani ya Victoria "Victoria garden" hivi karibuni, yamebainisha mafanikio ya serikali katika kukamilisha misingi hiyo muhimu ya utawala bora.

Kipimo cha kutambua dhamira ya kweli ya kutekeleza utawala bora, kinaweza kuonekana kwenye katiba ya nchi. Katiba ya Zanzibar ya Mwaka ya 1984 ambayo ndio msingi wa maamuzi yote ya kisheria kwa wananchi, inaelekeza wajibu wa wananchi katika kulinda mali ya Zanzibar na dhima yao katika kushiriki kwenye mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na viongozi mbali mbali na wananchi waliohudhuria sherehe za Maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu Duniani, wakiwa wamesimama wakati wimbo wa Taifa ukiimbwa. Maadhimisho hayo yamefanyika katika viwanja vya Victoria Garden Mjini Unguja, tarehe 10 Disemba, 2016

Katiba hiyo imeweka wazi wajibu wa kila mtu katika kufuata na kutii Katiba na Sheria za Zanzibar, kuchukua hatua za kisheria kama zilivyowekwa na kuhakikisha hifadhi ya Katiba na Sheria za nchi.

Watu wote wanatakiwa na sheria kulinda vizuri mali ya Zanzibar na kwa pamoja kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Zanzibar kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadae ya Taifa lao. Kila Mzanzibari ana wajibu wa kulinda, kuhifadhi kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa Zanzibar.

Katika kuimarisha utawala bora, viongozi wanapaswa kuhakikisha kwamba wanatoa taarifa sahihi na za kuaminika kwa wanaostahiki kwa wananchi na watu waliochini ya dhamana zao. Ni ukweli uliowazi kwamba wapo baadhi ya viongozi wanaodhani kwamba wanapohimizwa kutoa taarifa kwa wananchi, wanahimizwa kutangaza sera za vyama vyao na kamwe hawafahamu kwamba kutoa taarifa kwa wananchi ni wajibu wa Kikatiba kama inavyoelezwa katika Ibara ya 18 Kifungu (2)

”Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii”.

Licha ya kwamba Serikali imeweka utaratibu maalum unaowataka viongozi wa Serikali katika ngazi mbali mbali wawe wanatoa taarifa kwa wananchi, bado wako wanaodharau agizo hili kwa sababu mbali mbali zinazoambatana na utashi wao binafsi. “Wito wangu kwenu viongozi ni kuhakikisha mnatoa taarifa za kutosha kwa wananchi kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyopo. Utoaji wa taarifa ni msingi muhimu katika kuimarisha maadili kazini na kukuza utawala bora”. alisema Dk. Shein

Kwa upande mwengine serikali imekamilisha uundaji wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo imepewa mamlaka ya kusimamia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Tume hii hivi sasa imeshaanza kutoa elimu kuhusu umuhimu wa maadili.

Moja kati ya jukumu kubwa la Tume hii ni kuhakikisha kwamba viongozi wa umma na wale wote waliotajwa na Sheria ya maadili Na. 4 ya mwaka 2015 wanajaza na kuwasilisha fomu ya tamko la rasilimali na madeni zilizotolewa hivi karibuni kwa viongozi wote wanaotajwa na sheria hiyo. Ni jukumu la kila muhusika kuhakikisha kuwa anarejesha fomu hiyo kabla ya wakati uliopangwa kumalizika.

Kila mmoja ahakikishe anatoa taarifa za kweli katika kujaza fomu hiyo, taarifa zote zitakazotolewa ziwe sahihi kwani kujaza taarifa za uongo ni kosa kwa mujibu wa sheria hiyo.

Aidha, ni wajibu wa kila kiongozi kuyafahamu majukumu ya Tume hiyo na kutoa ushirikiano unaohitajika katika kutekeleza majukumu yake. Tume

imepewa majukumu kadhaa kwa mujibu wa sheria iliyounda tume hiyo ikiwa ni pamoja na kupokea na kuhifadhi tamko la taarifa za mali na madeni linalowasilishwa na kiongozi wa umma, kupokea tuhuma na taarifa za uvunjwaji wa maadili kutoka kwa wananchi na kufanya uchunguzi juu ya madai au tuhuma za uvunjwaji wa maadili dhidi ya kiongozi yeyote wa umma.

Vile vile ni jukumu la Tume kuchunguza mwenendo wa kiongozi yeyote wa umma ikiwa kwa lengo la kulinda uvunjwaji wa maadili. Kadhalika, kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu madai yoyote ya uvunjwaji wa maadili pamoja na kuelimisha umma juu ya umuhimu wa maadili.

Tume hii imepewa uwezo kisheria kumtaka mtu yeyote au taasisi yoyote kutoa au kuwasilisha taarifa au kujibu maswali na kuwasilisha kumbukumbu au nyaraka zozote zinazohusiana na tuhuma zinazohitaji kufanyiwa uchunguzi. Kadhalika, imepewa uwezo wa kuchunguza akaunti yoyote ya benki ambayo Tume inataka kujiridhisha kuhusu hesabu zake, hesabu za hisa, hesabu za manunuzi au nyaraka zozote zinazohusiana na akiba au amana.

Akizungumza katika maadhimisho ya sherehe za siku ya maadili zilizofanyika katika bustani ya Victoria, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ametoa wito kwa kila kiongozi aliyetajwa kwa mujibu wa sheria hiyo kuwa tayari kutoa mashirikiano yatakayohitajika ili kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Dk. Shein amesema Serikali imedhamiria kuondoa migongano ya maslahi kwa viongozi mbali mbali, kwani ina madhara makubwa kwa maendeleo na ustawi wa wananchi na kubwa zaidi wananchi kukosa imani kwa Serikali yao.

”Viongozi mna wajibu wa kuitii miiko ya uongozi, ikiwa ni pamoja na kujiepusha na ulevi wa kupindukia, uasharati, uropokwaji, utoaji wa siri, uzembe na kutojali matatizo ya wananchi, kushindwa kutunza familia na wazee wake, kushirikiana na watu wenye mienendo isiyokubalika, kushindwa kulipa madeni, kutumia kauli na lugha isiyofaa, ugomvi, udhalilishaji wa kijinsia, utapeli, wizi, ubakaji na vitendo vibaya, pamoja na kauli za kibaguzi zinazosababisha mgawanyiko wa kijamii, kiitikadi na kimaeneo”.

Serikali imeshatekeleza wajibu wake lakini jukumu kubwa lililombele ya jamii ni namna ya kutekeleza sheria hizo kwani kuwa na sheria ni jambo moja lakini kutekeleza na kuzisimamia sheria hizo ni jambo jengine tofauti. Kila mtu anawajibika kwa upande wake katika kufanikisha jukumu hili muhimu.

Kwa mfano dhana ya kuendeshwa uchumi wa nchi kwa makini na kushiriki katika vita dhidi ya uhujumu wa uchumi iliyozungumzwa kwenye Katiba, inajumuishwa na wajibu wa wananchi kuwafichua na kuwachukulia hatua watu wanaodai rushwa katika utoaji wa huduma, wizi wa mali za Serikali na taasisi binafsi, waharibifu wa miundombinu, watoro kazini, wategeaji na wazembe wa aina zote.

Kuwepo kwa vitendo vya uhujumu wa uchumi na rushwa katika taasisi za serikali zinazoshughulikia usimamizi na ukusanyaji wa mapato pamoja na utoaji wa huduma kwa wananchi bado ni tatizo linaloathiri ubora wa huduma, kipato cha wananchi na maendeleo ya nchi kwa jumla. Ili kukomesha vitendo hivi, kila mmoja anapaswa kushiriki kikamilifu katika vita hivyo kwa mujibu wa nafasi yake.

Wananchi hawanabudi kuwa tayari kuwaripoti bila ya woga wala huruma wale wote wanaojihusisha na vitendo hivyo. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) hainabudi kuendeleze kasi ya Mapambano dhidi ya Rushwa na uhujumu wa uchumi.

Aidha, Mamlaka hiyo hainabudi kuongeza bidii katika kutoa taaluma kwa jamii kuhusiana na dhana nzima ya mapambano dhidi ya rushwa. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa upande wake, vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi wanatakiwa kuendelea kwa kasi na ari zaidi kutoa ushirikiano unaohitajika ili Mamlaka hii ifanye kazi zake ipasavyo hasa kwa vile serikali imeshatangaza kuwa haitamuonea huruma mtu yoyote atakayebainika kushiriki katika vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa uchumi ikiwa ni pamoja na kufanya hujuma za miundombinu.

4

SMZ ilivyodhamiria kuinua huduma za jamii Mgonjoni

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali Maalim Abdalla Mzee wakati alipotembelea Ujenzi wa Skuli mpya ya Sekondari katika Kijiji cha Mgonjoni Wilaya ya Kaskazini B Unguja kuangalia ujenzi wa Skuli ya hiyo, tarehe 04 Disemba, 2016

Wakati mataifa mengi ya Bara la Afrika yakiwa yanaendelea kukabiliana na tatizo kubwa la umasikini vijijini huku baadhi yao yakiendelea kukabiliwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe na hali mbaya ya ukame, Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imo katika hatua za mwisho za kumaliza hali mbaya ya umasikini vijijini kwa kuvipatia huduma muhimu za kijamii vijiji vichache vya aina hiyo vilivyosalia.

Taarifa ya Wizara ya Afya zinasema kuwa yapo maeneo machache vijijini ambayo bado yanakabiliwa na tatizo la huduma za afya na kwamba huduma hiyo kwa sasa kwenye vijiji vingi inapatikana na wananchi kwenye umbali usiozidi masafa ya kilomita tano kutoka kwenye maeneo yao wanayoishi.

Kadhalika juhudi za kuimarisha miundombinu ya elimu katika awamu tofauti za uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea baada ya Mapinduzi, zimeifanya sekta hiyo ya elimu kupata mafanikio makubwa kama ilivyo sekta ya maji, umeme na bara bara.

Ni dhahiri upatikanaji wa maji safi na salama umeimrika zaidi kwenye vijiji vingi vya Unguja na Pemba kutokana na juhudi maalum zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya awamu ya saba kufuatia kuongezeka visima vilivyochimbwa hivi karibuni chini ya ufadhili wa serikali ya Rasulkhaima na Serikali ya Japan kupitia shirika lake la JICA.

Lakini pamoja na mafanikio hayo, vipo baadhi ya vijiji vichache ambavyo wananchi wake bado wanaendelea kuishi maisha ya shida kutokana na sababu mbali mbali. Moja kati ya vijiji vinavyoweza kupigiwa mfano kwa sasa ni kijiji cha Mgonjoni, Shehia ya Kilombero, Jimbo la Kiwengwa, Wilaya ya Kaskazini B, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Bonde kubwa la Mpunga la Kilombero limekitenga kijiji hiki na vijiji vingine na kulazimisha wakaazi wa Mgonjoni kutembea kwa miguu masafa marefu kutokana na kukosekana barabara na hata njia inayoweza kupita gari hasa wakati wa mvua.

Wakaazi wapatao 223 wa kijiji hiki hawanufaiki sana na mafanikio ambayo wananchi wengi wa Zanzibar wamekuwa wakijivunia baada ya kujitawala. Wakaazi wa kijiji cha Mgonjoni ni wakulima waliohamia kutoka kijiji cha Kijini, Matemwe miaka mingi iliyopita ikiwa ni katika harakati zao za kujitafutia maisha. Shughuli kuu za kiuchumi zinazofanywa na wananchi wa kijiji hiki ni kilimo na ufugaji.

Maisha ya wananchi wa kijiji cha mgonjoni yanaonekana kuwa ni duni

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja Mhe. Vuai Mwinyi Mohamed wakiangalia kisima kiliopo katika kijiji cha Mgonjoni Wilaya ya Kaskazini B Unguja ambacho Wananchi wakijiji hicho hujipatia huduma ya maji kwa matatizo makubwa na usumbufu

na yanafananishwa na yalivyokuwa maisha ya wananchi wa Micheweni kiasi ya miaka 15 iliyopita, kabla ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo kuchukua juhudi maalum kukabiliana na tatizo la umasikini katika kijiji hicho, ambacho tafiti zilionesha kuwa Wilaya ya Micheweni ndiyo Wilaya inayoongoza kwa kuwa na kiwango kikubwa cha umasikini ikilinganishwa na Wilaya nyengine zote za hapa Zanzibar.

Inawezekana katika shehia hii watu ni masikini zaidi kuliko Micheweni, lakini umasikini huo hauwezi kuonekana katika ngazi ya Wilaya kutokana na ukweli kwamba maeneo mengine ndani ya Wilaya hiyo hayako vibaya.

Huduma ya elimu ni moja kati ya changamoto kubwa kwa watoto, walezi na wazazi wa kijiji cha Mgonjoni. Kwa muda mrefu wananchi wa Mgonjoni wamekuwa wakilazimika kufuatilia huduma ya elimu masafa yasiyopungua kilomita 3.5 katika skuli ya Kilombero kutokana na kukosa skuli ya kusomea kwenye kijiji chao.

Lakini tatizo la masafa linaonekana kuwa ni dogo kuliko mazingira yenyewe ya kufuata masomo. Wakaazi wa kijiji hiki hulazimika kukatisha kwenye bonde la mpunga la Kilombero ambalo kwa wakati wa mvua hasa za masika inakuwa vigumu kwao kupita.

Hali hiyo inawafanya wanafunzi wanaoishi kwenye kijiji hicho kushindwa kwenda skuli wakati wa mvua au wanapofika wanakuwa wameroa na kuweko katika mazingira magumu siyo tu ya kuweza kusoma, lakini pia namna ya kukaa na wenzao wakavu darasani. Hali inakuwa mbaya pia wakati wanaporudi kijijini kwao kutoka skuli ambapo vile vile hukabiliwa na mvua au jua kali.

Ukosefu wa huduma ya maji safi na salama, umeme, barabara na ukosefu wa kituo cha afya ni changamoto nyengine kwa wananchi wa kijiji hiki. Wananchi wa Mgonjoni hulazimika kufuata huduma ya afya katika kijiji cha Upenja kilichoko umbali wa kilomita 8.5.

Huduma ya maji inapatikana kutoka kwenye kisima kimoja, ambacho inasemekana ni kimoja kati ya visima virefu zaidi hapa Zanzibar. Huduma ya maji hupatikana kwa kuchotwa kwa kutumia ndoo inayofungwa kamba refu na kuchelezwa kisimani humo.

Baada ya dhiki faraja, ni msemo maarufu wa Kiswahili wenye kumaanisha neema baada ya dhiki/shida ya muda mrefu. Wananchi wa kijiji cha Mgonjoni kwa ushirikiano na uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Serikali ya Wilaya ya Kaskazini B, wamefanikiwa kupata ufadhili kukabiliana na changamoto ya elimu inayokikabili kijiji hicho.

Kupitia ufadhili huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika hatua za awali inajenga skuli ya kisasa ya maandalizi na msingi itakayokuwa na madarasa manne (4), ambayo kwa mujibu wa idadi ya wakaazi wa kijiji cha Mgonjoni yanatosha kukidhi mahitaji ya sasa ya kijiji hicho.

Kijiji cha Mgonjoni kina jumla ya wanafunzi 28 wanaosoma skuli ya Kilombero na wanafunzi 37 wanasoma kijijini hapo katika kituo cha maandalizi cha tucheze tujifunze. Wanafuzni 14 miongoni mwao wamemaliza elimu ya maandalizi kijijini hapo katika kituo kilichowekwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alifanya ziara maalum ya kukitembelea kijiji hicho ili kujionea mwenyewe hali halisi ya kijiji hicho na anakuwa Rais wa kwanza wa Zanzibar kukitembelea kijiji hiki tokea wananchi wa kijiji hicho walipohamia miaka mingi iliyopita.

Katika ziara yake hiyo aliyoifanya Disemba 3, 2016, alifanya mazungumzo na wananchi wa Mgonjoni na kuwaahidi kuwa serikali inazifanyia kazi changamoto zote zinazowakabili na kuwahakikishia kuwa ufumbuzi wake hautachukua muda mrefu.

Dk. Shein ambaye katika ziara yake alifuatana na viongozi mbali mbali wa taasisi za serikali, Mheshimiwa Mbunge na Muwakilishi wa jimbo la Kiwengwa, aliwaagiza viongozi na watendaji wa sekta zote zinazohusika na changamoto zilizotajwa kuwakabili wananchi wa kijiji hicho kuzitafutia ufumbuzi wake haraka iwezekanavyo.

Ameipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuamua kujenga skuli ya maandalizi na msingi ambayo inatarajiwa kuanza kazi mwezi Januari mwaka 2017. Dk. Shein amewaahidi wazazi, walezi na wanafunzi wa skuli hiyo kuwapatia huduma zote za skuli bure ikiwemo sare, chai ya asubuhi na

Matukio mbali mbali katika Picha

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipokea zawadi kutoka wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu,pia Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Prof.Suleiman Bin- Nassry Basahal wakati wa sherehe ya Mahfali ya kumi na nne iliyofanyika katika Chuo hicho huko Tunguu Wilaya ya Kati Unguja, tarehe 07 Disemba, 2016

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi zawadi Mhitimu Samiya Suleiman Seif, ambaye amefanya vizuri zaidi katika masomo yake katika sherehe ya Mahfali ya kumi na nne (14) ya Chuo Kikuu cha Tunguu (Zanzibar University) kilichopo Tunguu Wilaya ya Kati, tarehe 07 Disemba, 2016

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipatiwa maelezo na Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar Ndugu Abdalla Malimosi wakati alipotembelea kituo kidogo kinachofanyiwa matengenezo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume akiwa katika ziara maalum, tarehe 04 Disemba, 2016

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipeana mkono na Mkuu wa Mkoa Mstaafu Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis kama ishara ya kumkabidhi gari mpya ya Noah iliyotolewa na Ofisi ya Mkoa Mjini Magharibi katika sherehe za kumpongeza mstaafu huyo kwa Utumishi wake katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hafla hiyo imefanyika katika ukumbi wa zamani wa Baraza la Wawakilishi Mnazi Mmoja Mjini Unguja, tarehe 31 Disemba, 2016

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akifanya mahojiano na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) Ndugu Aiman Duwe katika ukumbi wa Ikulu Mjini Unguja, tarehe 31 Disemba, 2016

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akiwa na wake wa viongozi mbali mbali na wananchi katika sherehe za maadhimisho ya Maulid ya kuzaliwa Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) zilizofanyika katika Viwanja vya Maisara Mjini Unguja, tarehe 12 Disemba, 2016

5

Mama Mwanamwema apongeza mpango wa SMZ wa kuwasaidia wazee

Mama Mwanamwema Shein, Mke wa Rais wa Zanzibar

Heshima kwa wazazi na wazee ni jambo lililopewa umuhimu wa aina yake katika maisha ya kila siku ya mwanadamu, na ni jambo lenye kumpa daraja kubwa mtu yeyote anayeonekana kulitekeleza akiwa hapa duniani.

Kwa kutambua umuhimu wa msemo maarufu wa kiswahili usemao “isiyokongwe haivushi”, mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein ameshindwa kuzuia hisia zake na kumpongeza hadharani Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuanzisha Pensheni Jamii kwa wazee wote wenye umri kuanzia miaka 70.

Mama Mwanamwema Shein ambaye alikuwa katika ziara yake ya kutoa shukurani na pongezi kwa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), kwa kuiwezesha CCM kuendelea kuongoza Serikali, alitoa shukurani kwa Dk. Shein kwa jinsi alivyothamini juhudi za wazee wa hapa nchini na hatimae kuwatengea pensheni hiyo.

Akieleza juhudi hizo, Mama Shein ambaye alikuwa akizungumza katika ukumbi wa CCM Amani akiwa pamoja na viongozi mbali mbali wakiwemo wake wa viongozi na viongozi wengine wa chama na Serikali, alisema kuwa katika suala zima la kuthamini michango ya wazee, katika kipindi cha pili cha uongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Awamu ya Saba, chini ya Rais Dk. Ali Mohamed Shein, wananchi wanashuhudia jinsi Serikali inavyoongeza kasi katika kupanga na kutekeleza mipango yenye lengo la kuimarisha ustawi wa wazee.

Mama Shein alisisitiza kuwa miongoni mwa mambo ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatakiwa iyatekeleze kwa ajili ya wazee ni pamoja na kuhakikisha wazee wanatambulikana na kupatiwa huduma za matibabu bila ya malipo, kuhakikisha wazee wanapatiwa haki zao za kisheria na kupatiwa fursa sawa katika ngazi zote.

Serikali imekuwa ikiongeza juhudi katika kuhakikisha kuwa Serikali inawalinda wazee dhidi ya vitendo vya ukatili vikiwemo mateso na mauaji, kuwawekea miundombinu na mazingira bora yatakayowawezesha kwenda wanapotaka na kutumia vyombo vya usafiri wa umma kwa gharama nafuu pamoja na kuweka utaratibu utakaowawezesha wazee kulipwa pensheni.

Kwa kutambua umuhimu wa wazee katika kujenga misingi imara ya maendeleo hapa nchini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 iliandaa na kutekeleza mipango imara ya kuwatunza, kuwaenzi na kuwaendeleza wazee.

Juhudi hizo za Serikali ambazo zinatekelezwa hadi hivi leo pamoja na utamaduni wa Zanzibar unaohimiza kuwa na mapenzi na wazee kwa kuwatunza na kuwashirikisha katika mipango ya maendeleo na kifamilia, zimeifanya Zanzibar kuwa ni miongoni mwa nchi bora katika bara la Afrika inayotekeleza vyema maisha ya uzeeni.

Mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliwajengea wazee nyumba za makaazi, Unguja na Pemba kwa ajili ya kuwaenzi na kuwatunza pamoja na kuwapa huduma muhimu bila ya malipo mambo ambayo hadi leo yanaendelezwa.

Ni faraja ilioje kuona Serikali imeanza kutekeleza kwa ufanisi mkubwa mpango wake wa kuwapatia pensheni maalum wazee wote wa Unguja na Pemba waliofikia umri wa miaka 70 bila ya kujali historia ya kazi walizokuwa wakizifanya, wakati huo huo serikali ikielezea azma yake ya kutaka kuongeza fedha hizo na kupunguza umri, ikifikiria uwezekano wa kuwaingiza wazee kuanzia umri wa miaka 65.

Hata hivyo, inasikitisha pia, kuona baadhi ya watendaji wanafanya udanganyifu katika zoezi hilo kwa kuwaingiza baadhi ya watu waliokuwa hawana sifa, katika orodha za wazee wanaostahiki kupata malipo na kuwaacha wenye sifa, jambo ambalo lilionesha kumkasirisha siyo tu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, lakini pia liliwakasirisha na wengine wengi wenye kupenda haki na maendeleo ya Zanzibar.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Wazee alipowasili katika sherehe za maadhimisho ya siku ya Wazee Duniani zilizofanyika Wilaya ya Chake chake katika viwanja vya nje Uwanja wa Gombani Mkoa wa Kusini Pemba, tarehe 01 Oktoba 2016

Akiwahutubia wananchi katika hafla ya Kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani, iliyofanyika Gombani, Wilaya ya Chake, Mkoa wa Kusini Pemba, Rais wa Zanzibar aliiagiza Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kulishughulikia tatizo hilo na kuwachukulia hatua watendaji wote walioshindwa kuwajibika na ambao wamelisababisha tatizo hilo.

Kauli mbiu ya siku ya wazee ya mwaka huu ilinasema ‘Chukua hatua, dhidi ya unyanyasaji wa wazee” ilikwenda sambamba na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mapambano dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia, udhalilishaji watoto na vitendo vyote vya ukatili katika jamii.

Pongezi za Mama Shein kwa Rais wa Zanzibar hazikutolewa kwa upendeleo. Jitihada za Rais wa Zanzibar kwa wazee zinastahiki kupongezwa na kila mtu na hasa mpenda maendeleo. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Dk. Shein imefanya juhudi kubwa pia katika kulishughulikia suala la kiinua mgongo kwa wafanyakazi wa Serikali waliostaafu.

Mnamo mwezi Machi 2016, kiasi cha Tsh. Bilioni 16.2 zilitolewa kwa ajili ya kuwalipa watu viinua mgongo na wengi walifaidika hasa wale waliotaka kwenda Hijja. Hapa inazungumziwa watu waliostaafu ambao wanaelekea uzeeni.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imo katika mchakato wa kuwapatia vitambulisho maalum wazee ili viweze kuwasaidia katika kupata huduma muhimu za kijamii.

Pensheni jamiii itasaidia kuondoa umasikini na inatekeleza malengo endelevu yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa ambapo nchi zote duniani zimeamua kutekeleza hatua hiyo muhinu itayohakikisha afya na maisha bora kwa wazee.

Masuala ya wazee Zanzibar yalianza kushuhulikiwa kabla ya tamko la Umoja wa Mataifa kwani hatua za kuwatuza wazee na kuwasaidia ilianza rasmi mara baada ya Mapiduzi ya 1964 chini ya uongozi wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.



Hadhi ya Karafuu ilivyorejea Zanzibar

Mafanikio ya harakati za maisha ya binadamu hupimwa kutokana na jinsi alivyoondokana na mambo yasiyokubalika katika jamii na kujikita katika mambo yanayokubalika siyo tu katika jamii, lakini pia katika ile miongozo iliyotolewa na muumba katika vitabu vyake vitukufu.

Ni katika misingi hii, hata wale waliofanikiwa kuwa na fedha nyingi au kupata utajiri mambo ambayo wengi wanayakimbilia, hawataonekana kuwa wamefanikiwa iwapo watakuwa na tabia au mambo machafu yasiyokubalika kwa muumba na katika jamii wanayoishi.

Mara nyingi jamii imekuwa ikiwaheshimu watu ambao wanaonesha ubinadamu mbele ya wenzao hasa kwa kuwawekea wenziwao mambo ya msingi ambayo yanawasaidia katika maisha yao ya kila siku lakini hata baada ya maisha yao ya hapa duniani. Ni wazi kwamba wenye kufanya hayo wanalo fungu kubwa kwa Muumba kama ilivyoelezwa kwenye vitabu vya Mwenyezi Mungu.

Hii hasa ndio sababu watu wengi wenye uwezo na wenye kulifahamu hili, huwa hawachelei kuwaanzishia miradi ya kuwaendeleza wananchi kiuchumi, kuwajengea skuli na madrasa, nyumba za ibada na mambo mengine ya aina hiyo bila ya kuhitaji ujira wowote kutoka kwa wanaofanyiwa hayo.

Uamuzi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wa kulirejeshea hadhi zao la karafuu ambalo kimsingi lilishaanza kupotea katika orodha ya mambo yanayochangia uchumi wa Zanzibar, unaweza kuhesabiwa miongoni mwa mambo ambayo yamemletea sifa kubwa hapa duniani na bila ya shaka faida yake ataiona kesho huko sote twendako.

Ni ukweli usiopingika kwamba Serikali na wakulima wa karafuu Unguja na Pemba walishapoteza imani na zao hilo na wapo wengi walioamua kuikata mikarafuu yao na kuitumia kwa matumizi mengine yasiyojali zao hilo.

Hakuna aliyetamani kupanda mkarafuu miaka 7 au 8 iliyopita, lakini wapo wengi waliodiriki kuikata na kuchoma makaa, kuni au kujengea wakiamini kuwa mti huo unawaka vizuri unapotumiwa kwa matumizi ya kuni, una makaa mazuri unapofanywa makaa, na pia una sifa za

kipekee unapojengewa kwani hakuna mdudu anayeutamani kuula kama wanavyofanya mchwa kwenye aina nyengine za miti.

Kwa kufahamu kwamba karafuu hasa zile za Zanzibar zina sifa ya pekee kwenye soko la dunia, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein iliyaona manufaa ambayo wananchi hasa wakulima wa karafuu wanaweza kuyapata kiuchumi kutokana na zao hilo, iwapo mazingatio maalum yatafanywa kuwasaidia.

Ingawa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa miaka mingi imekuwa ikilitambua na kulithamini zao la karafuu kuwa ndilo zao lake kuu la kiuchumi ndani na nje ya nchi, kulikuwa na wakati ambapo viongozi Serikalini walitofautiana kuhusiana na hatma ya zao hilo; wapo waliotaka zao hilo libinafsishwe kutokana na kukumbwa na misukosuko katika soko la ndani na pia kwenye soko la kimataifa. Lakini wapo waliosema hapana wakiamini kwamba mawazo hasi "negative" yaliyopo kuhusiana na zao hilo, yanaweza kugeuzwa na kuwa chanya "positive" iwapo hatua madhubuti na za makusudi zitachukuliwa na serikali.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ndiye aliyekuwa ameshika kinara akiongoza kundi la wanaoamini kwamba zao hilo ambalo kwa mujibu wa historia ya uchumi wa Zanzibar ndio muokozi wa uchumi kwa wanyonge na taifa kwa jumla, alisema haiwezekani zao hilo kubinafsishwa, inawezekana serikali kuleta mabadiliko kwenye zao hilo na kujenga taswira tofauti na iliyopo wakati huo takriban miaka sita (6) iliyopita.

Bila ya shaka msimamo wa Dk. Shein katika suala hilo ulizingatia ahadi yake aliyokuwa ameitoa kwa wananchi alipokuwa akiomba kwao ridhaa ya kuongoza katika kipindi cha kwanza cha uongozi wake kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010.

Dk. Shein amefanikiwa kutekeleza ahadi nyingi alizoziahidi wakati wa kampeni zake za uchaguzi za mwaka 2010-2015, lakini moja ya ahadi ambazo ilionekana kuwa haiwezi kutekelezeka na kuonekana kuwa ni maneno ya kujitafutia kura, ni ile ya kuliimarisha zao la karafuu. Wako wengi waliokuwa wakibeza na kukebehi ahadi hiyo wakichukulia kuwa ilikuwa mzaha na ni mchezo wa kisiasa.

Katika hatua zake za mwanzo, serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dk. Shein ilipitisha uamuzi wa kulifanyia mabadiliko makubwa Shirika la Biashara la Taifa ZSTC kwa kulifanya shirika hilo sio tu kujiendesha kibiashara lakini pia kupata ufanisi mkubwa katika shughuli zake.

ZSTC lilianza kutekeleza mageuzi yake mwaka 2011/2012 na ndipo ulipoanza kuonekana uwezekano wa Shirika hilo kujiendesha kwa tija kwa wakulima, wenye mashamba ya mikarafuu na wananchi ambao watahusika kwa njia moja au nyengine katika shughuli za karafuu.

Baada ya serikali kuridhika na mageuzi hayo na kiutendaji, mwezi Disemba 2011 kiasi cha mwaka mmoja tu baada ya kuingia ofisini rasmi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alitia saini sheria mpya ya ZSTC Nam. 11 ya mwaka 2011 inayotoa Mamlaka

na uwezo kwa shirika hilo kulisimamia, kulihudumia, kuliimarisha zao la karafuu na kuhakikisha kuwa linakuwa endelevu kwa maslahi ya wakulima, wananchi na taifa kwa jumla.

Mafanikio ya wakulima yalionekana wazi mara baada ya kutangazwa bei mpya ya karafuu ambayo ni kutoka bei ya zamani ya shilingi 5,500 kwa kilo moja hadi shilingi 15,000. Asilimia 80 ya mauzo ya karafuu inarejea kwa wakulima moja kwa moja na asilimia 20 kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja, ambapo Serikali hutumia fedha hizo kuimarisha huduma za jamii kama vile matibabu, elimu, maji safi na salama na mengineyo mambo ambayo pia yanarudi kwa wananchi.

Hatua ya serikali ya kuongeza bei ya karafuu kwa wakulima ilirejesha moyo mpya kwa wakulima kuanza kuyafufua mashamba yao, kuyatunza na kuyalinda wakati wote kinyume na kipindi kirefu kilichopita ambacho mkulima wa karafuu hakuweza kuona thamani ya mikarafuu yake kutokana na karafuu zenyewe kukosa soko na hivyo kupelekea kudharaulika mashamba ya mikarafuu.

Sambamba na hatua hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kushirikiana na ZSTC imeanzisha kampeni maalum ya kupanda mikarafuu miche 1,000,000 kila mwaka na kuigawa kwa wakulima bure.

Uamuzi wa serikali wa kuongeza bei ya karafuu haikuwa mwisho wa jitihada za serikali za kulirejeshea hadhi zao hilo. Hatua ziliendelea kuchukuliwa za kuliendeleza zao hilo kwa kuanzisha mfuko maalum wa karafuu ambao madhumuni yake makubwa ni kuwaendeleza wakulima wa karafuu nchini ili kuona wanapiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu umeanzishwa kwa mujibu wa sheria Namba 2 ya mwaka 2014 chini ya kifungu Namba 4 ambacho kinaipa mamlaka Bodi ya Shirika la ZSTC kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya karafuu. Mfuko huo ambao upo chini ya Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la ZSTC, unaendesha shughuli zake kwa ufanisi kutokana na kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo, ruzuku na misaada kwa wadau wa karafuu yaani wakulima, wamiliki mashamba na wakodishwaji.

Hatua hizo na nyingi nyenginezo kama vile kuimarisha huduma za ununuzi wa karafuu, kujenga barabara kwenye maeneo yenye karafuu nyingi, kutoa miche ya mikarafuu kwa wakulima, kutafuta masoko ya nje na kuwatia moyo wakulima wa zao hilo kwa kuwapatia mikopo wakulima hao kumekuwa kukitoa msukumo wa kuliendeleza zao hilo.

Kutokana na juhudi zote hizo wadau wa sekta ya zao la karafuu, wakulima na wananchi wengi hasa wale wanaoishi katika maeneo yanayozalishwa karafuu wamekuwa wakitoa maoni yao yenye mnasaba wa kuipongeza serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kutokana na juhudi zake anazoendelea kuchukua ambazo kwa kweli sasa zimesharejesha hadhi na ubora wa karafuu ya Zanzibar.

Hakika juhudi za serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za awamu ya saba katika kulirejeshea hadhi zao la karafuu ni za kupigiwa mfano.

Bw. Khamis Issa Mohamed ni mmoja wa wadau wa sekta ya zao la karafuu Zanzibar, amesema kuwa jitihada kubwa zinazochukuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia shirika lake la ZSTC katika kuliimarisha zao la karafuu na kuweza kulirejeshea hadhi na heshma yake zaidi ya ilivyokuwa hapo nyuma, zinastahili kupongezwa na kuungwa mkono na wadau wote wa zao la karafuu.

"Naipongeza serikali kwa kuongeza bei nzuri ya karafuu na kuwajengea mazingira mazuri wakulima wa zao hilo na hasa kwa uanzishwaji wa Mfuko wa maendeleo ya karafuu hatua ambayo inasaidia sana uimarishaji wa sekta hiyo muhimu" alisema Bw. Khamis.

Mkulima mwengine wa zao hilo mkaazi wa Mkarafuuni Mkoani Mohamed Juma Makame alisema kuwa bei iliyowekwa na serikali katika kipindi cha uongozi wa Dk. Shein haijawahi kutokea hivyo kwa kuthamini juhudi hizo wataendelea kushirikiana na shirika la ZSTC kwa kuhakikisha kwamba wanaendelea kuuza karafuu zao katika shirika hilo.

"Ni kawaida ya baadhi ya binadamu kuwa na tamaa binafsi ya kipato na mimi nawashangaa sana watu wanaoendesha biashara za magendo ya karafuu kwani hatma ya kazi hiyo ni hasara au majuto baadae" alisema Mohamed Juma.

Ukweli usiofichika kwamba baada ya kubaini kwamba Serikali tayari imejiimarisha katika eneo hilo, wapinga maendeleo wamekuwa wakichoma mashamba ya mikarafuu kwa kufahamu kwamba kufanya hivyo kunaweza kudhoofisha uchumi wa nchi na wananchi wake. Aidha, jamii nayo imekuwa ikiwalaani wale wote wanaofanya vitendo ambavyo hatimaye vinapelekea kulihujumu zao la karafuu.

Zao la karafuu Zanzibar sasa limepata mwelekeo mpya kutokana na kuweko usimamizi mzuri wa kuitunza mikarafuu ya zamani na kuisimamia mikarafuu midogo iliyoanza kupandwa na yote yenye umri kati ya mwaka mmoja hadi miaka sita.

Ukweli mtazamo wa wananchi na serikali kuhusu karafuu kwa ujumla sasa uko chanya na sio hasi kama ilivyokuwa miaka saba au minane iliyopita.



7

“Tusivifumbie macho vitendo vya udhalilishaji” Mama Mwanamwema Shein

Mama Mwanamwema Shein, Mke wa Rais wa Zanzibar

Vilio vinavyotokana na vitendo vya udhalilishaji vimekuwa vikisikika na kusambaa nchini kote kutoka kwa wananchi, viongozi wakuu wa kitaifa, jumuiya na taasisi mbali mbali za serikali na watu binafsi kutokana na athari kubwa za kijamii na kisaikolojia zinazowapata wanaothirika na vitendo hivyo.

Ni dhahiri kwamba vitendo hivyo havipaswi kufumbiwa macho katika jamii kama ya Watanzania ambayo inaamini misingi ya haki na usawa kama inavyoainishwa katika kifungu cha 12, kifungu kidogo cha 2 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na katika kifungu cha 11, kifungu kidogo cha 2 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kisemacho “Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.”

Kwa mnasaba huu, jamii inapaswa kuuona ukweli huo na haipaswi kuwepo mtu wa kumdhalilisha mtu mwengine kwa sababu yoyote. Vibaya zaidi inapotokezea kumdhalilisha mtoto mdogo kwa sababu tu ya kukosa uwezo na nguvu za kufahamu na kukataa kitendo afanyiwacho, mwanamke kwa sababu tu ya jinsia yake, maumbile yake na huruma yake, au dhana potofu ya kumuona kuwa yeye ni mtu dhaifu.

Ni vyema ikafahamika na kila mmoja kwamba kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutokana na jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria kama ilivyoelezwa kwenye katiba ya Zanzibar na vile vile katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Imeelezwa katika katiba ya Zanzibar Ibara 15 (i) kwamba Kila mtu anastahiki kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na ya nyumbani kwake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake.

Ni ukweli uliowazi kwamba, kwa mujibu wa vifungu hivyo vya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na sheria nyengine za haki za binadamu zilizokuwepo nchini na zile za kimataifa, vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto ni uvunjaji mkubwa wa haki za binadamu na haki za kikatiba. Hivyo, lazima jamii yote ichukue hatua madhubuti na kutekeleza dhamira ya kuendeleza utawala bora wenye kutoa heshima kwa nchi yetu.

Jitihada za Zanzibar katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto ni za muda mrefu kwani tayari Zanzibar imeshapitisha sheria ya kuwalinda watoto wa kike dhidi ya kupewa uja uzito ambayo inatoa adhabu ya kifungo kwa waliotiwa hatiani.

Katika mwaka 2011, ilipitishwa sheria ya mtoto (Sheria Nam 6 ya mwaka 2011) ambayo nayo inalenga kuwalinda watoto. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa sera ya maendeleo ya wanawake na sera ya

hifadhi ya maendeleo ya watoto kama miongozo mikuu katika kusimamia masuala yanayowahusu wanawake na watoto.

Sheria na sera hizo zote zinatoa nguvu za kisheria na miongozo ya kujenga mazingira mazuri ya kukuza ustawi wa wanawake na watoto, ikiwa ni pamoja na kusimamia vyema upatikanaji wa haki zao za msingi. Hata hivyo, ufanisi wa suala hili utafikiwa iwapo kila mmoja na kila taasisi itatimiza wajibu wake katika kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wake imeshaonesha dhamira yake ya kutekeleza suala hilo kwa kuchukua hatua za kuzirekebisha sheria kila inapobidi kufanya hivyo kwa lengo la kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto vinadhibitiwa.

Takwimu zilizokusanywa katika vituo vya mkono kwa mkono vilivyoko katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Wete, Chake chake na Koteji za Makunduchi, Kivunge na Micheweni zinaonesha kuwa kati ya mwaka 2011 hadi mwezi Juni 2014 jumla ya matukio 2,415 yameripotiwa katika vituo hivyo.

Matukio 2,669 yalihusu watoto wa kike na 164 ya watoto wa kiume. Matukio hayo yanahusisha vitendo vya kunajisi, kubaka, uja uzito na kuwatorosha watoto walio chini ya uangalizi wa wazee wao. Miongoni mwa waathirika wa matukio hayo wamo wafanyakazi wa majumbani na watu wenye ulemavu.

Kadhalika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na taasisi ya Action Aid mwaka 2012, wanawake 36 katika kila wanawake 100 katika Mkoa wa Kaskazini Unguja wamekiri kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kimwili ikiwemo kupigwa na kuunguzwa. Hali hii haitowi taswira nzuri hasa kwa wanaume. Inapaswa kila wakati kukumbuka msemo mashuhuri wa wahenga kwamba, “Mke hapigwi kwa fimbo, hupigwa kwa mapambo”.

Utafiti unaelezea zaidi kuwa Wanawake 17 kati ya 100 waliohojiwa kwa upande wa Unguja na wanawake 33 kati ya 100 waliohojiwa katika Kisiwa cha Pemba, wamekiri kuwa wamefanyiwa ukatili wa kulazimishwa kufanya mapenzi.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa kutoka Dawati la Jinsia Makao Makuu ya Polisi Zanzibar, matukio 1,210 ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake yameripotiwa katika vituo vya polisi kuanzia mwaka 2010 hadi mwezi Agosti, mwaka 2014.

Ni wazi kuwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake huondoa mapenzi na kupunguza huruma waliyo nayo kina mama kwa wanaume na vile vile kwa watoto jambo ambalo halipaswi kufurahiwa.

Taarifa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinaeleza kuwa kesi 149 za wanafunzi waliopewa ujauzito kati ya mwaka 2010 hadi mwaka 2014 kutoka Wilaya kumi za Zanzibar zimeripotiwa.

Aidha, katika kipindi hicho kuna matukio 229 ya wanafunzi waliokatishwa masomo yao na kuozeshwa waume. Kesi hizo zinawahusu watoto kuanzia darasa la nne hadi kidato cha nne na ni zile zilizoripotiwa tu lakini huenda ziko zaidi ya idadi hiyo. Hii siyo taarifa nzuri hasa wakati huu ambapo serikali imekuwa ikichukua juhudi maalum kuimarisha sekta ya elimu nchini.

Jamii hainabudi kuzinduka na kuangalia ilikotoka ambako misingi bora ya malezi na kufuata maadili na mafundisho ya dini ni miongoni mwa mambo muhimu yaliyokuwa yakitumika katika kukabiliana na vitendo vyote vya mmong’onyoko wa maadili, ikiwemo udhalilishaji wa watoto na wanawake.

Pamoja na kuwepo kwa changamoto zinazotokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani, ni dhahiri kwamba bado jamii yetu ina wajibu wa kuwalea watoto kwa kuzingatia silka, mila, desturi na utamaduni, ikiwemo kushirikiana katika malezi na kuona kuwa mtoto wa mwenzio nawe ni wako.

Akizungumza katika mikutano tofauti ya kinamama hivi karibuni, Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein amewataka kinamama na watanzania wote kwa jumla kuendelea kuhimizana na kuuendeleza utamaduni wa malezi ya pamoja na kuzingatia maadili ya nchi, kwani alisema utamaduni huo na maadili ya nchi ni mkakati bora wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa watoto.

“Napenda nitoe wito kwa viongozi wa dini, wanasiasa, viongozi wa vyombo vya habari na viongozi wa taasisi za kiraia na jumuiya zisizo za kiserikali, kuzidi kuelimisha wananchi kwa njia mbali mbali juu ya athari na ubaya wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa mujibu wa dini, sheria na utamaduni na umuhimu wa kushirikiana katika kupambana navyo”. Alisema.

Mama Mwanamwema alielezea kusikitishwa kwake na vitendo hivyo vya udhalilishaji hasa pale inapotokezea kwamba taarifa za kesi hizo zinawahusisha watu wa karibu na watoto waliofanyiwa vitendo hivyo, wenye uhusiano wa damu, au waliopewa dhamana ya ulezi wa watoto hao, jambo ambalo ni kinyume na maadili na kamwe halikubaliki katika jamii.

Uzoefu unaonesha kuwa hali kama hii mara nyingi husababisha kesi zake kuishia kinyume na matarajio ya wengi kwa sababu ya kuoneana muhali na wahusika huachiwa huru bila ya kuzingatia sheria na hivyo kuwaacha walioathirika kubaki na ulemavu, unyonge na machungu ya kisaikolojia muda wote wa maisha yao duniani.

“Wito wangu kwenu nyote, tuseme sasa na iwe basi. Tusemeni kwa maneno na kwa vitendo. Tuanze ukurasa mpya katika kuzindua kampeni hii. Watu wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, wapelekwe kwenye vyombo vya sheria, na tushirikiane katika kutoa ushahidi bila ya kumuonea mtu”. Alisema Mama Mwanamwema Shein.

Ni ukweli ulio wazi kuwa suala hili limekuwa changamoto kubwa kwa wazazi wengi. Katika kukabiliana na changamoto za namna hii jitihada za pamoja baina ya serikali, taasisi zisizokuwa za serikali, jumuiya za kiraia na taasisi za kidini zinahitajika.

Aidha, ni vyema ikakumbukwa kwamba familia ni chuo cha mwanzo cha maadili, tabia na mwenendo bora wa mtoto. Hivyo, wazazi na walezi wanabeba uzito wa pekee katika kupiga vita vitendo hivyo kwa kufuatilia kwa karibu nyendo za watoto wao.

Ni dhahiri kuwa kufanikiwa kwa kampeni hii ya kukabiliana na ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto kutategemea sana juhudi za pamoja katika kuimarisha mikakati ya kukabiliana na suala hili.

8

Mabadiliko ni hatua ya lazima Zanzibar

Ngoma ya Kibati ikichezwa na kikundi cha vijana cha Ngoma Group katika sherehe za maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu Duniani zilizofanyika katika viwanja vya "Victoria Garden" Mjini Unguja, tarehe 10 Disemba, 2016

"Kulikoni na ongezeko la matukio ya udhalilishaji wa wanawake na watoto Zanzibar?"; Hili ndilo suala ambalo Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein na watu wengine wenye busara, hekima na wenye kuifahamu vilivyo historia, utamaduni na asili ya Zanzibar na watu wake wamekuwa wakijiuliza bila ya kupata jibu.

Taarifa kutoka kwa watu mashuhuri, vitabu, machapisho na hotuba za viongozi zinaonesha kuwa Zanzibar ni moja kati ya visiwa vyenye sheria nyingi nzuri. Miongoni mwa sheria hizo zimo zile zilizokuwa zikitumika tokea wakati wa ukoloni, sheria zilizotolewa kama amri au matamko ya viongozi na nyengine zilizopitishwa kwenye Baraza la Wawakilishi. Baadhi ya sheria hizo zimefanyiwa marekebisho ili ziende sambamba na wakati uliopo.

Lakini moja kati ya sheria ambayo imeipa sifa kubwa Zanzibar kitaifa na kimataifa, ni sheria ya watoto ya Zanzibar ya mwaka 2011. Kutokana na ubora wa sheria hiyo, taasisi ya kimataifa "World Future Council" ilitoa tunzo maalum kwa Zanzibar (Gold Future Policy Award) kwa mwaka 2015.

Tunzo hiyo ilikuwa ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wake wa ndani na nje katika kuimarisha haki na ustawi wa watoto nchini kupitia sera, sheria na mikakati ya utekelezaji wake.

Zanzibar kwa muda mrefu ilijijengea sifa ya kuwa na maadili mema kwa watu wake na hasa watu kuheshimiana. Hili limethibitishwa na wazee mbali mbali wa Unguja na Pemba katika mazungumzo yao na mwandishi wa makala hii.

Historia inatufundishi kuwa Zanzibar hakukuwa na malezi ya mtu mmoja mmoja. Jamii ilishirikiana katika malezi ya watoto. Haikuwa kosa bali ilikuwa kawaida kwa mzee yeyote kumrudi au kumuadabisha mtoto wa mtu mwengine pale anapofanya au anapoelekea kufanya kosa lililokithiri au jambo linalokwenda kinyume na maadili. Mfumo huo wa malezi ya watoto ndio uliotoa watu wenye nidhamu na maadili mazuri.

Kwa bahati mbaya hii imebaki kuwa historia. Katika zama hizi linakuwa kosa kubwa kwa mtu asiyekuwa baba au mama kumchukulia hatua za kinidhamu mtoto aliyetenda kosa ambaye siye mwanawe. Lakini haishangazi kuona kwamba sheria ambayo imetufanya tupate tunzo ya dhahabu nayo inapinga vitendo hivyo vya kuwaadabisha watoto wetu. Imeshashuhudiwa mara kadhaa wazazi kufikishwa mahakamani kwa kuwaadabisha watoto wao waliowazaa. Sheria za kimataifa zinakataza aina na malezi tuliowalea watoto wetu. Baadhi wanahoji; Je! hivi ni kweli utandawazi ndio unaotufanya kupoteza mila na desturi zetu?

Zanzibar kwa muda mrefu ilikuwa chimbuko la walimu na maulamaa ambao wamewafundisha watu wengi

misingi ya dini ya kiislamu ndani hadi nje ya nchi. Dini ya kiislamu na dini nyengine zote zinakataza maasi yote yanayomchukiza Muumba ikiwemo vitendo vya udhalilishaji. Kwa bahati mbaya, taarifa kutoka vyombo mbali mbali vya habari zinaonekana kuwahusisha zaidi walimu wa madrasa katika matukio hayo ambayo siyo tu yamekatazwa na Muumba, lakini yanachukiza sana ndani ya jamii. Je! Ni kitu gani kimewakuta watu hawa waliokuwa wakiheshimika sana kwenye jamii yetu?

Taarifa zinaonesha kuwa kama kuna kipindi ambacho wanasheria wengi wamehitimu kutoka vyuo mbali mbali Zanzibar, basi ni kipindi cha miaka kumi iliyopita. Ni kipindi hicho ambacho serikali imeajiri wanasheria wengi zaidi kuliko kipindi chochote kilichopita. Hivi karibuni, Jaji Mkuu wa Zanzibar aliwaapisha mawakili wapatao 117, ambao bila ya shaka wamefikia vigezo vya kuwa mawakili. Sambamba na hatua hiyo, ofisi kadhaa za mawakili wa kujitegemea zimefunguliwa.

Katika hali ya kawaida kutokana na mabadiliko hayo, mtu angetarajia kuona ufanisi mkubwa wa masuala yote ya kisheria ikiwemo kuharakisha maamuzi ya kesi zote zikiwemo za udhalilishaji wa wanawake na watoto. Kwa bahati mbaya, tatizo la ucheleweshaji wa kesi mahakamani limekuwa sugu wakati huu kuliko wakati mwengine wowote. Je! Nini kimetokea kwenye mahakama zetu na kwenye fani hii ya sheria?

Serikali kwa upande wake imefanya juhudi kubwa za kufundisha wataalamu wa fani mbali mbali pamoja na kupata mabingwa wa tiba ya afya. Ni fahari kubwa kwa serikali kusema inayo mabingwa na maabara za kisasa na hivyo kuwa rahisi kuweza kubaini mambo mbali mbali. Kwa bahati mbaya, huu ndio wakati unaofanywa mambo ya ajabu yanayohitaji uthibitisho wa madaktari lakini yanashindikana. Inashangaza kusikia watu wanaokamata unga unaodhaniwa kuwa madawa ya kulevya, unapofikishwa kwa mkemia mkuu kuthibitishwa, unabainika kuwa haikuwa madawa ya kulevya bali yalikuwa ni majivu, ambayo aliwekwa binaadamu tumboni akiyasafirisha kutoka nchi za mbali.

Jeshi la polisi nalo limesheheni mabingwa katika upelelezi wa makosa

Mtumiaji wa dawa za kulevya akijidunga sindano, vitendo hivi ni kinyume na maadili na huathiri vijana wengi ambao ndio nguvu kazi ya taifa

makubwa ya jinai kutoka ngazi ya chini hadi kufikia Kamishna. Karibuni kwenye maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi tumeshuhudia mbwa wenye uwezo mkubwa wa kutambua wahalifu pengine ni zaidi kuliko uwezo alionao binadamu katika baadhi ya masuala. Kwa bahati mbaya, huu ndio wakati unaoingizwa dawa nyingi za kulevya nchini kuliko wakati wowote na athari yake inaonekana kila mahala. Bahati mbaya zaidi kwamba hakuna taarifa zinazozungumzia kukamatwa kwa wanaofanya biashara hizo wala wanaotiwa hatiani kwa makosa hayo kama ilivyo kwa wanaokamatwa na kutiwa hatiani kwa makosa mengine kama vile wizi wa mazao, ubakaji na kuwatorosha wasichana wenye umri chini ya miaka 18.

Vipo visingizio kwamba maendeleo ya sayansi na teknolojia yanachangia vitendo hivyo kwa misingi kwamba mambo ambayo yalikuwa yakifanywa kwa siri miaka ya nyuma hivi sasa yanafanyika dhahiri. Vile vile kuna dhana kwamba mila na desturi zetu zimeingiliwa na wageni na kwa kujua au kwa bahati mbaya tumekuwa tukifuata mkondo huo.

Ni ukweli uliowazi kwamba bado maswali yanakuwa mengi kuliko majibu kuhusiana na namna jamii na vyombo vya sheria wanavyolishughulikia suala la kusimamia sheria za nchi kwa ujumla wake na hasa udhalilishwaji wa wanawake na watoto.

Utaratibu uliokuwa ukitumika zamani wa kuwalipia nauli na posho watu ambao walikuwa wakitoa ushahidi mahakamani umeondolewa jambo ambalo limekuwa likiwavunja moyo wanaopaswa kutoa ushahidi.

Inawezekana pia kwamba misaada ya wafadhili ambayo inaambatana na masharti maalum imekuwa ikituondoa katika maadili yetu bila ya kujua na baadhi ya wakati imekuwa ndio chanzo cha mifarakano katika jamii.

Jambo lililowazi kabisa ambalo linaonekana na kila mtu ni kuporomoka kwa maadili, ubinafsi, kukosa uzalendo pamoja na kutowajibika ipasavyo katika majukumu yetu ya kazi lakini pia katika jamii.

Ufumbuzi wa kujitoa tulipofikia ni kubadilika na kuacha kufanyakazi kwa mazowea. Hata hivyo, utaratibu wa kubadili mwenendo wa maisha ya mwanadamu ni mchakato ambao huchukua muda mrefu. Pamoja na hayo, dhamira ya kweli katika kuleta mabadiliko hayo ndiyo itakayoweza kuijenga Zanzibar mpya yenye maadili mazuri, uzalendo na hisia ya kuleta maendeleo endelevu kwa jamii ya Wazanzibari wote na Tanzania kwa jumla na sio kwa mtu mmoja mmoja. Inawezekana tutimize wajibu wetu.

9

Pemba washuhudia kasi mpya ya Dk. Shein

■ Wamekiri kuwa yeye ndiye chaguo la Wazanzibari

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akiwasalimia Wananchi wakati alipotembelea Ujenzi wa Barabara ya Mgagadu - Kinanzini yenye urefu wa Kilomota 7.6 katika Wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba alipofanya ziara ya kutembelea barabara hiyo tarehe 07 Novemba, 2016

Minong'ono na uvumi kuhusu kurejewa uchaguzi mkuu wa Zanzibar mambo ambayo yalizagaa kisiwani Pemba, yanaonekana kufikia tamati baada ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kuweka bayana kwa wananchi wa Pemba taratibu za kikatiba kuhusiana na suala la uchaguzi mkuu wa Zanzibar.

Akiwa anakaribia kutimiza mwaka mmoja tokea Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilipomtangaza rasmi kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufuatia kushinda katika uchaguzi wa marudio uliofanyika tarehe 20 Machi 2016 na kumpa ushindi wa asilimia 91.4, Dk. Shein amewabainishia wananchi wa Pemba kwamba uchaguzi umeisha na kilichobaki sasa ni kwa kila mmoja kufanya kazi za kuwaletea maendeleo yao na taifa lao.

Tokea kumalizika kwa uchaguzi huo kulikuwa na minong'ono kutoka kwa baadhi ya wanasiasa wa vyama vya upinzani na wafuasi wao, ambao wamekuwa wakipoteza muda wao mwingi kusambaza taarifa zisizokuwa za kweli kwa wananchi kwa kutumia njia mbali mbali zikiwemo za mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi.

Tarehe 5 hadi 9 Novemba 2016, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alifanya ziara kisiwani Pemba na kupata nafasi ya kuzungumza na viongozi wa serikali, chama tawala CCM na wananchi wa maeneo mbali mbali yakiwemo ya Micheweni, Chake Chake na Mkoani kisiwani Pemba, ambapo aliwabainishia wananchi kwamba uchaguzi umekwisha na amewataka kuzipuuza taarifa za baadhi ya wanasiasa wanaoeneza maneno ya mitaani kwamba kutakuwa na uchaguzi

mwengine ambao utabadilisha serikali iliyoko madarakani na viongozi wake wote.

"Uchaguzi umekwisha na mimi ndiye Rais halali wa Zanzibar na Mwenyeikiti wa Baraza la Mapinduzi, zipuuzeni taarifa za kurejewa uchaguzi. Uchaguzi mkuu mwengine utafanyika mwaka 2020. Endeleeni kufanya kazi zenu za kujiletea maendeleo yenu kwa bidii" alisisitiza Dk. Shein.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo na mimi ndiye Rais. Ni serikali halali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na wala hakuna nchi, taasisi iwe ya ndani au ya nje yenye uwezo wa kuiondoa serikali hii madarakani wala kuhoji uhalali wa uwepo wake". alisisitiza Dk. Shein kwa wananchi hao.

Katika ziara yake hiyo Dk. Shein amewatoa wasi wasi wananchi ambao walikuwa wakidhani kwamba kunaweza kutokea nchi au taasisi ambayo ingeweza kutengua uhalali huo wa serikali iliyochaguliwa na wananchi waliowengi katika Visiwa vya Unguja na Pemba kama ambavyo imekuwa ikizungumzwa na wanasiasa wa upinzani kwa wafuasi wao.

Wito wa Dk. Shein wa kuwataka wananchi kuendelea kufanyakazi zao badala ya kukaa vibarazani na kwenye maskani kuhubiri siasa umekuja wakati muafaka, ambapo serikali imeshafanyakazi kubwa ya kuweka mazingira bora ya kazi katika sekta zote muhimu kiuchumi kwa kuweka miundo mbinu yote muhimu kama vile maji, umeme na mawasiliano mambo ambayo yanarahisisha shughuli za kilimo, biashara, uvuvi na ufugaji na kwamba kilichobaki sasa ni wananchi wenyewe kujituma.

Kwa upande wa Kilimo, serikali tayari imeshafanya juhudi kubwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na inayoendelea hivi sasa, na ni vyema wananchi wakatumia fursa zilizopo ili waweze kunufaika na mazao bora yatayotokana na kilimo cha kisasa.

Serikali imeshapitisha sera na sheria kadhaa kwa lengo la kuimarisha sekta hiyo ya kilimo lengo likiwa kuweka mazingira bora zaidi kwa wakulima ambao mchango wao ni mkubwa katika pato la taifa. Miongoni mwa sera na sheria zilizopitishwa ni pamoja na Sera ya Masoko na bidhaa za kilimo ambayo tayari imeanza kutumika, Sheria ya kuanzishwa kwa taasisi ya utafiti wa Kilimo Zanzibar na Sheria ya Haki Miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Pamoja na juhudi hizo, Serikali katika kipindi hiki imedhamiria kuongeza uzalishaji wa zao la karafuu pamoja na uzalishaji wa mazao mengine ya chakula na biashara hususan manjano, hiliki, tangawizi, pilipilimanga, kungumanga, kilimo cha alizeti na kuanzisha mazao mengine mapya.

Ni dhahiri kwamba mafanikio ya utekelezaji wa mipango hiyo kwa kiasi kikubwa yanahitaji kuungwa mkono na wananchi waliokubali kujituma kufanyakazi kwa bidii na siyo kukaa vibarazani kuhubiri siasa, mambo ambayo yameshapitwa na wakati.

Kwa upande wa wajasiriamali, serikali imechukua juhudi maalum kuwawekea wananchi mazingira mazuri ya kujiendeleza kibiashara kwa kufanya mambo mbali mbali ikiwemo

Mkurugenzi wa Mfuko wa Barabara katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Nd. Ali Twahir akitoa maelezo kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakati alipotembelea Ujenzi wa Barabara ya Mgagadu - Kinanzini yenye urefu wa Kilomota 7.6 katika Wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba alipofanya ziara ya kutembelea barabara hiyo, tarehe 07 Novemba, 2016

kuimarisha mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuweza kumudu kuwakopesha wajasiriamali na wafanyabiashara wengi zaidi.

Aidha, serikali imekiimarisha kituo cha kulelea wajasiriamali kilichoko Mbweni, ambacho idadi ya wajasiriamali wanaojiunga na chuo hicho imekuwa ikiongezeka siku hadi siku. Mipango inafanywa na serikali ili kuhakikisha kuwa kituo kama hicho kinajengwa kisiwani Pemba siku chache zijazo.

Fursa zinapatikana pia katika ufugaji ambako serikali inahimiza ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa na nyama, mbuzi pamoja na kuku wa nyama na mayai ili kuongeza tija na kipato cha wafugaji kwa kutekeleza mambo mbali mbali ikiwemo kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ili kuwekeza katika sekta ya mifugo na viwanda vya usindikaji wa mazao ya mifugo sambamba nakuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi wa sekta ya mifugo.

Kadhalika, kwa wananchi walioamua kujituma fursa zinapatikana katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini. Kutokana na kutambua kuwa uvuvi na uzalishaji wa mazao ya baharini ni miongoni mwa shughuli muhimu za kiuchumi zinazofanywa na wananchi wengi wanaoishi pembezoni mwa mwambao wa bahari, serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanya mambo mengi yanayoonekana wazi wazi yakilenga kuwasaidia wananchi kukabiliana na changamoto ya umasikini.

Kwa kushirikiana na Taasisi ya Sayansi ya Baharini "Institute of Marine Science – IMS" na kampuni ya ununuzi wa mwani ya Birr, utafiti ulifanywa juu ya uwezekano wa kulima mwani aina ya "kotonii" kwenye kina kirefu cha maji huko Fundo, Shumba Mjini, Mkia wa Ng'ombe, Tumbe na Makangale Pemba na kubaini mafanaikio mazuri. Jumla ya tani 51,687 zenye thamani ya shilingi bilioni 18.7 zimezalishwa na kusafirishwa nchi za nje.

Ili kuwaendeleza wakulima wa mwani, jumla ya vihori 100 vilitolewa kwa njia ya mkopo kwa vikundi 50 vya wanawake wanaolima mwani, jambo ambalo pia linathibitisha dhamira ya kweli ya serikali kuwaendeleza kiuchumi wananchi wake.Kama hiyo haitoshi, katika kipindi hiki serikali imedhamiria kuendelea kununua vihori 500 vya kubebea mwani na kuvisambaza kwa wakulima wa mwani 3,000 Unguja na Pemba ili kuongeza uzalishaji wa mwani.

Hizi ni fursa chache tu kati ya nyingi ambazo wananchi wanaweza kuzitumia kuendeleza maisha yao badala ya kuendelea kukaa kuzungumzia masuala ya siasa ambayo mwisho wa siku hayatakuwa na faida yoyote kwao wala kwa taifa.